

HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI

(Barua zote zianzidikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)

Email: ded@babatidc.go.tz



S. L. P. 400,
BABATI.

Kumb. Na. DED/BBT/B.30/20/65

04.09.2018

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya Babati Kupitia kibali cha ajira mbadala kilichotolewa kwa barua kumb Na. FA170/448/01/85 cha tarehe 20 Julai 2018, Nakupitia kibali cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango, anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa kuomba nafasi za kazi kama ifuatavyo:-

A: DEREVA DARAJA LA II - NAFASI MOJA (01) AJIRA YA KUDUMU-NAFASI HII IMERUDIWA KUTANGAZWA

NAFASI TATU (03) AJIRA YA MUDA/MKATABA

Sifa za kuajiriwa:

- Mwombaji wa nafasi hii awe na ufaulu wa kidato cha nne
- Awe na leseni ya daraja la "C" au "E" ya uendeshaji wa magari yote
- Awe na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua mwaka mmoja (01) bila kusababisha ajali,
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari yanayotolewa na chuo cha VETA; NIT au chuo kingine kinachotambuliwa na serikali.
- Mwenye cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II atakuwa na sifa ya kufikiriwa kwanza
- Awe na umri usio chini ya miaka 18 na usiozidi miaka 45

B: KAZI ZA KUFANYA:-

- Kuendesha magari ya abiria na malori
- Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote na kufanya ukaguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo,
- Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari
- Kutunza na kuandika daftari la safari " Log – book" kwa safari zote
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake wa kazi

Mshahara:

Kwa kuzingatia ngazi za mshahara za watumishi wa Umma **TGS B.**


MAMBO MUHIMU YA KUZINGIATIA KWA WAOMBAJI WOTE:-

- (1) Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Babati na nje ya Halmashauri ya Wilaya Babati.
- (2) Barua za maombi ziambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu, Taaluma, Cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi (Passport size) za hivi karibuni
- (3) Barua za maombi ziambatanishwe na maelezo binafsi ya mwombaji (CV)
- (4) Testimonials " Provisional Results", "Statement of results", hati za matokeo za kidato cha nne au sita (FORM IV RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA
- (5) Waombaji waliosoma nje ya nchi, waambatanishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA).

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **19/09/2018 saa 9:30 Alasiri.**

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Babati,
S.L.P. 400,
BABATI.


Hamisi Iddi Malinga
**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BABATI**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI**